

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA KUMI

YATOKANAYO NA KIKAO CHA NANE

08 FEBRUARI, 2018

MKUTANO WA KUMI

KIKAO CHA NANE TAREHE 08 FEBRUARI, 2018

I. DUA

Saa 3:00 Asubuhi Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika alisoma Dua na kuongoza Bunge.

MAKATIBU MEZANI:

1. Ndg. Stephen Kagaigai
2. Ndg. Nenelwa Wankanga
3. Ndg. Lawrence Makigi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

- (a) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu) - Mhe. Jenista J. Mhagama aliwasilisha Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevyya ya Mwaka 2016;
- (b) Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria - Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017;
- (c) Mhe. Esther Mmasi K.n.y Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017;
- (d) Mhe. Maidah Abdallah K.ny Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati hiyo kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliuliza maswali:-

- | | | |
|-----------------------------------|---|---------|
| (a) Mhe. Richard Mganga Ndassa | - | CCM |
| (b) Mhe. Margareth Simwanza Sitta | - | CCM |
| (c) Mhe. Devota Methew Minja | - | CHADEMA |
| (d) Mhe. Zubeir Mohamed Kuchauka | - | CUF |
| (e) Mhe. Balozi Diodorus Kamala | - | CCM |

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 99 Mhe. Flatei Gregory Massay

Nyongeza (i) Mhe. Flatei Gregory Massay
 (ii) Mhe. Mashimba Ndaki
 (iii) Mhe. Deo Sanga

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Swali Na. 100 Mhe. Boniphace Mwita Getere

Nyongeza (i) Mhe. Boniphace Mwita Getere
 (ii) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga
 (iii) Mhe. Alex Raphael Gashaza

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na. 101 Mhe. Mwantumu Dau Haji

Nyongeza (i) Mhe. Mwantumu Dau Haji

- (ii) Mhe. Joyce John Mukya
- (iii) Mhe. Dkt. Prudensia Wilfred Kikwembe

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 102 Mhe. Hamad Salim Maalim

- Nyongeza
- (i) Mhe. Hamad Salim Maalim
 - (ii) Mhe. Jaku Hashim Ayub

WIZARA YA MADINI:

Swali Na. 99 Mhe. Anna Joram Gidarya

- Nyongeza
- (i) Mhe. Anna Joram Gidarya
 - (ii) Mhe. John Constantine Kanyasu
 - (iii) Mhe. Ruth Hiyob Mollel

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na. 103 Mhe. Deogratias Francis Ngalawa

- Nyongeza
- (i) Mhe. Deogratias Francis Ngalawa
 - (ii) Mhe. Jesca David Kishoa

WIZARA YA NISHATI:

Swali Na. 104 Mhe. Neema William Mgaya

- Nyongeza
- (i) Mhe. Neema William Mgaya
 - (ii) Mhe. Hussein Nassor Amar
 - (iii) Mhe. Lucy Simon Magereli
 - (iv) Mhe. Daniel Nicodamus Nsanzugwanko
 - (v) Mhe. Hamidu Hassan Bobali

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Swali Na. 105 Mhe. Juma Ali Juma

Nyongeza (i) Mhe. Juma Ali Juma
 (ii) Mhe. Hassan Elias Massala

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 106 Mhe. Lathifa Hassan Chande

Nyongeza (i) Mhe. Lathifa Hassan Chande
 (ii) Mhe. Juma Selemani Nkamia
 (iii) Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete

V. MATANGAZO:

(A) WAGENI

1. Wageni 11 wa Mhe. Jenista J. Mhagama – Waziri wa Nchi.
2. Wageni 41 wa Mhe. Fatma Hassan Toufiq ni Viongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kutoka Wilaya Saba za Mkoa wa Dododma wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Ndg. Faustine Sabugo.
3. Wageni 2 wa Mhe. Josepher F. Komba ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwalubunge Ndg. Mwanahamisi Shabani na Katibu wa Kata ya Kicheba, Ndg. Musa Kopwe kutoka Muheza Mkoani Tanga.
4. Wageni 32 wa Mhe. Anthony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ni Wajumbe wa

Halmashauri Kuu ya CCM – Tawi la Reli kutoka Mkoani Dodoma.

5. Wageni 4 wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza ni Viongozi wa Rusumo Fans Hydroelectric Power Project kutoka Ngara Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Meneja Biashara Ndugu Huang Liang.
6. Mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mch. Johanis Salufu - Mwenyekiti wa Wazazi Wilaya ya Kilolo.
7. Wageni 6 wa Mhe. Pauline Gekul ni Viongozi wa Halmashauri ya Mji wa Babati na Wazee kutoka Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mhe. Mohamed Kibiki.
8. Wanafunzi 75 na Walimu 15 wa Shule ya Sekondari ya Wasichana St. Monica ya Jiji la Arusha.
9. Wanafunzi 95 na Walimu 3 kutoka Shule ya Sekondari ya Kigwe ya Mkoani Dodoma.
10. Wanafunzi 54 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Mkoa wa Dodoma.

(B) MATANGAZO MENGINE

1. Mhe. Suleiman Ali Yussuf aliwatangazia Wabunge wote Waislamu wakutane saa 7.00 mchana baada ya kusitisha shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Anex Dispensary.
2. Mhe. Maftaha A. Nachuma alimtangaza Mhe. Kiza Mayeye kama Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya CUF badala ya Mhe. Abdallah Mtalea kutokana na uchaguzi uliofanywa na Carcus ya CUF.

3. Naibu Spika alitoa ufanuzi kuhusu utaratibu wa Maswali ya Msingi na Nyongeza kwamba lazima uzingatie Kanuni ya 38 – 46.
4. Naibu Spika aliondoka na kumwachia Kiti Mwenyekiti Mhe. Andrew John Chenge.

MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Hussein Mohamed Bashe alitumia Kanuni ya 47 kuomba Hoja ya Dharura ili Bunge ijadili juu ya uhaba wa maji katika Jimbo la Nzega ambapo kwa sasa hakuna maji kabisa mpaka Mbunge kugharamikia maboza kufikisha maji katika Jimbo hilo la Nzega;
2. Mwenyekiti alitoa nafasi kwa Serikali kuweza kutoa majibu. Mhe. Jenista Mhagama (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu) aliomba Mawaziri wa Maji, Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Bashe wakutane ofisini kwake yeye Waziri wa Nchi ili kuona namna ya kushughulikia tatizo hilo la maji.
3. Mhe. Juma Nkamia alitumia Kanuni ya 68 (7) kuomba mwongozo kuhusu Mradi wa Maji katika Wilaya ya Kondoa na Chemba, kwamba alipouliza swali kuhusu fedha ya maji shilingi bilioni mbili iliyopelekwa kwa ajili ya maji kwa Wilaya hizo ililiwa na Watendaji na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi yao na badala yake wamehamishwa na Waziri alipojibu swali lake alisema Serikali itapeleka fedha ili Wananchi wapate maji na kuacha wabadhilifu huru.

Mwenyekiti alijibu mwongozo huu kuwa; ni vyema Mbunge azingatie Kanuni na Msingi uliowekwa kwani swali la Mhe. Nkamia halikuwa la msingi. Hivyo anaweza kuleta swali hilo kama swali la msingi ili ajibiwe vizuri.

4. Mhe. Flatei Gregory Massay alitumia Kanuni ya 68 (7) kuomba Mwogozo kwamba swali lake Na. 99 kuhusu Mji Mdogo wa Hydom halikujibiwa ipasavyo.

Mwenyekiti alijibu kuwa atakwenda kujiridhisha kwa kupitia majibu yaliyopo kwenye hansard na kama majibu hayajitoshelezi atatoa mwongozo wake.

5. Mhe. Halima Mdee aliomba mwongozo wa Spika, kuhusu kuridhiwa kwa Hoja ya Mhe. Bashe kwamba Bunge lijadili Hoja ya Dharura kwa kuwa tatizo la maji limekuwa ni kubwa mno na kila Mbunge akisimama huongelea changamoto hiyo ya maji.

Mwenyekiti alijibu kuwa; ni kweli tatizo ni kubwa kiasi ambacho hoja hiyo yaweza kulitoa Bunge kwenye ratiba yake. Hivyo Bunge livute subira ili Mawaziri wakakae halafu walete majibu Bungeni. Pia Wabunge waweze kujadili jambo hili katika Kamati za Kisekta.

6. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma alitumia Kanuni ya 68 (7) kuhusu Kamata kamata ya Wananchi wavua samaki na kuacha wavuvi haramu wakivua samaki jambo ambalo limesababisha kifo cha mvuvi mmoja kilichotokana na njaa. Na kwamba swalii hili liliulizwa juzi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi alitoa majibu mepesi.

Mwenyekiti alijibu kuwa jambo hili halijatoka mapema leo, isipokuwa Serikali imesikia hilo hivyo Serikali isipuuze malalamiko ya Wananchi.

7. Mhe. Ridhiwan Kikwete alisimama kwa Kanuni ya 68(7) na alilalamikia kutojibiwa vyema kwa swalii lake kuhusu changamoto ya maji katika Jimbo lake la Chalinze, na kwamba Waziri alimwambia analeta siasa, jambo ambalo siyo kweli kwani uhaba wa maji Chalinze umepelekea hata kiwanda cha Sayona kufungwa.

Mwenyekiti alijibu kwamba; kwa kuwa swalii la Mhe. Ridhiwan halikuwa swalii la Msingi ila lilitokana na swalii la msingi la Mhe. Lathifa, basi ni vyema sasa Mhe. Ridhiwan alete swalii hilo kama swalii la msingi apate majibu mazuri.

8. Mhe. Susan Kiwanga alitumia Kanuni ya 68(7) kuhusu panya wanaokula mazao ya wananchi katika Mashamba ya Kilombero na kuleta hatari ya njaa katika maeneo hayo. Vilevile Mhe. Waziri na

Mkurugenzi wa Wilaya, walienda na wanafahamu tatizo la panya lakini mpaka leo hakuna sumu ya kuua panya hao iliyopelekwa.

Mwenyekiti alijibu, kwamba Serikali yaweza kutoa majibu, lakini suala hilo halijatokea Bungeni mapema leo.

9. Mhe. Mussa Mbarouk aliomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) alisema katika swali lake Na. 105 hakupata majibu mazuri kwani transifoma iliyopelekwa Jimboni kwake haina nguvu kiasi cha kukwamisha hata miradi ya maji. Pia aliomba hoja ya maji ijadiliwe.

Mwenyekiti alisema sio vyema kuunganisha hoja ya maji na umeme, ila Serikali iseme kidogo kuhusu umeme.

10. Mhe. Waitara alitumia kanuni ya 68(7) aliomba Bunge lijadili hoja ya dharura kuhusu maji kwani naye alikuwa na hoja hiyo katika Jimbo lake la Ukonga na alimwalika Mhe. Waziri. Hoja ya kukaa Serikali na kuleta majibu sio sawa.

Mwenyekiti alijibu kuwa, japo hoja hii ya Ukonga haijatokea leo mapema ila ahadi ya Serikali itekelezwe.

11. Mhe. Pascal Haonga alitumia Kanuni ya 68 (7) kuwa Mawaziri wanapojobu Maswali husifia Wabunge wa CCM kuwa wao ni jembe lakini Wabunge wa Upinzani hawasifiwi. Hii ni kileta siasa Bungeni.

Mwenyekiti alisema, hakuna ubaya kusifu, wasiofanya vizuri wajitahidi kufanya vizuri nao wapewe sifa.

VI. HOJA ZA KAMATI:

1. Mhe. William Ngeleja aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

2. Mhe. Omary M. Mchengerwa aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.
3. Mhe. Jasson Rweikiza aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

VII. MAJIBU YA MIONGOZO ILIYOPITA

- (a) Mwongozo wa Mhe. Peter Serukamba kuhusu kutoridhishwa na majibu ya Swali Na. 96 swali la tarehe 7/2/2018 lililojibiwa na Wiziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.
- (b) Mwongozo wa Mhe. Pauline Gekul kuhusu kutoridhika na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa swali lake la nyongeza swali la tarehe 7/2/2018 ulijibiwa.

VIII. KUSITISHA BUNGE

Saa 7.20 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni.

IX. BUNGE KURUDIA

Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia na Wabunge wafuatao waliendelea kuchangia Taarifa za Kamati.

| | | | |
|-----|----------------------------------|---|---------|
| 1. | Mhe. Taska Restuta Mbogo | - | CCM |
| 2. | Mhe. Daniel Edward Mtuka | - | CCM |
| 3. | Mhe. Amina Saleh Mollel | - | CCM |
| 4. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | CCM |
| 5. | Mhe. Mwanne Ismail Mcemba | - | CCM |
| 6. | Mhe. Jumanne Kibera Kishimba | - | CCM |
| 7. | Mhe. Alfredina Apolinairy Kahigi | - | CUF |
| 8. | Mhe. Ester Michael Mmasi | - | CCM |
| 9. | Mhe. Khalifa Mohamed Issa | - | CUF |
| 10. | Mhe. Ruth Hiyob Mollel | - | CHADEMA |
| 11. | Mhe. Zacharia Paulo Issaay | - | CCM |

| | | | |
|-----|---|---|-----------------------|
| 12. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya | - | CCM |
| 13. | Mhe. Pascal Yohana Haonga | - | CHADEMA |
| 14. | Mhe. Suleiman Masoud Nchambi | - | CCM |
| 15. | Mhe. Godbless Jonathan Lema | - | CHADEMA |
| 16. | Mhe. Stella Ikupa Alex Ofisi ya Waziri Mkuu (Ulemavu) | - | Naibu Waziri |
| 17. | Mhe. Mhe. George Kakunda Waziri Mkuu (TAMISEMI) | - | Naibu Waziri Ofisi ya |
| 18. | Mhe. Suleiman Jafo ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) | - | Waziri wa Nchi, Ofisi |
| 19. | Mhe. Palamagamba John Kabudi na Sheria | - | Waziri wa Katiba |
| 20. | Mhe. George Huruma Mkuchika Utumishi na Utawala Bora | - | Waziri wa |
| 21. | Mhe. Jenista Joackim Mhagama Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Kazi, Ajira na Watu wenye | - | Waziri wa |
| 22. | Mhe. William Mganga Ngeleja Makamu Mwenyekiti Kamati ya Sheria Ndogo | - | |
| 23. | Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa wa Kamati ya Katiba na Sheria | - | Mwenyekiti |
| 24. | Mhe. Jasson Samson Rweikiza wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | - | Mwenyekiti |

Kuhitimisha Hoja

- (c) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria alihitimisha Hoja ya Kamati yake na kutoa Hoja kuliomba Bunge likubali kupitisha Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati yake;
- (d) Bunge lilihojiwa na kukubali Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati hiyo kuwa Maazimio ya Bunge;
- (e) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo alihitimisha Hoja ya Kamati yake na kutoa Hoja kuliomba Bunge likubali kupitisha Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati yake;

- (f) Bunge lilihojiwa na kukubali Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati hiyo kuwa Maazimio ya Bunge;
- (g) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa alihitimisha Hoja ya Kamati yake na kutoa Hoja kuliomba Bunge likubali kupitisha Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati yake;
- (h) Bunge lilihojiwa na kukubali Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati hiyo kuwa Maazimio ya Bunge;
- (i) Mwenyekiti aliwashukuru Wabunge kwa michango na Wenyeviti wa Kamati kwa Taarifa zote kuweza kuziwasilisha kwa wakati na kuagiza Serikali ifanyie kazi Maazimio yote yaliafikiwa na Bunge.

Matangazo:

- i. wageni wa Mhe. Nchambi walitambulishwa;
- ii. Taarifa ya Serikali kwa Mhe. Bashe ilitolewa na Mhe. Jenista Mhagama kuhusu tatizo la maji.

X. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 1. 30 Usiku Kikao cha Bunge kilahirishwa hadi tarehe 9/2/2018 saa 3.00 asubuhi.